# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 26 Eliya na Elisha

**SOMA 1 Wafalme 17 na 18:20 – 40 na 19:11 – 14; 2 Wafalme 5:1 – 19**

**SOMO**

*Baali*



Wafalme wote wa ufalme wa Israeli walikuwa waovu. Waliabudu miungu na waligeuza watu wa Israeli wasiabudu Mungu. Mungu alituma manabii kuwafundisha njia Zake kuwarejesha ili wamwabudu tena. Mmoja wa hawa wafalme waovu alikuwa Ahabu. Alifundisha watu kuabudu Mungu, Baali. Mungu alikasirika sana. Mungu alituma nabii Eliya kwa Ahabu. Eliya aliambia Ahabu kwamba Mungu hajafurahishwa na yeye kwa sababu alifundisha watu kuabudu Baali. Eliya alimwambia kwamba hakutakuwa na mvua nchini mpaka **Mungu** aseme ndiyo inyeshe.

Hakukuwa na mvua kwa muda mrefu na kukawa na njaa kwa nchi. Mungu alilinda Eliya. Alimwambia aende kuishi kwa kijito cha Kerithi. Eliya alikunywa maji kutoka kwa kijito. Mungu alituma kunguru wamletee nyama na mikate kwa midomo yao kila asubuhi na jioni akila.

Baada ya muda kijito kilikauka. Lakini Mungu aliendelea kulinda Eliya. Aliambia Eliya aende kwa mji wa Sarepta atapata mwanamke mjane atakayemlisha. Eliya alipofika Sarepta, alimkuta mwanamke akiokota kuni. Alimwomba maji na chakula. Alijibu Eliya kwamba kwa sababu ya njaa hakukuwa na chakula. Alimwambia kwamba alikuwa anaokota kuni ili aende apike chakula cha mwisho ale na mwanawe. Alikuwa na konzi ya unga kwa bakuli na mafuta kidogo kwa kopo. Baada ya hicho chakula watakufa.

Eliya aliambia huyu mjane amtengenezee chakula kidogo kwanza. Eliya alimwambia kwamba, Mungu atafanya unga na mafuta hayatakwisha kwa wakati wote wa njaa. Huyu mjane alikuwa na imani na akafanya vile Eliya alimwambia - na kulikuwa na unga na mafuta ya kutengeneza chakula chao vile Mungu alisema.

Siku moja mwana wa huyu mjane akakufa. Eliya alipeleka huyo mtoto kwa chumba chake na kumweka kwa kitanda chake. Eliya alijinyorosha kwa mtoto mara tatu akiomba Mungu. Mungu alimhuisha na akawa hai tena. Yule mwanamke alipoona hivyo, aliamini kwamba Eliya ni nabii wa Mungu na alikuwa na ukweli wa Mungu.

### Maswali na Majibu

1. Mungu alituma nabii gani kwa Ahabu mfalme muovu? *Eliya.*
2. Mbona Mungu alisema hakutakuwa na mvua?
   *Kwa sababu mfalme Ahabu na watu waliabudu Baali.*
3. Eliya alipata chakula namna gani kwa Kijito cha Kerithi na Sarepta?
   *Kunguru walimletea chakula kwa Kijito cha Kerithi. Kule Sarepta, mjane alimlisha kwa unga kidogo na mafuta yenye haikuisha.*
4. Eliya alionyesha namna gani kwamba Mungu ni Mungu wa kweli?
   *Mungu alituma moto kwa madhabahu ya Eliya. Baali hakutuma moto.*
5. Mungu alizungumzia Eliya namna gani alipokuwa anatoroka?
   *Alimzungumzia kwa sauti tulivu na ya chini.*
6. Nani alikuwa nabii baada ya Eliya? *Elisha.*
7. Elisha aliona nini wakati Eliya alichukuliwa kwa upepo ya kisulisuli?
   *Elisha aliona gari na farasi za moto.*
8. Elisha aliambia Naamani afanye nini ili apone kutoka kwa ukoma?
   *Aoge kwa Mto wa Yordani mara 7.*
9. Mbona Naamani alikasirika? Watumwa wake walifanya namna gani ndiyo akakubali?
   *Alijiona kwamba yeye ni mtu wa maana sana kuoga kwa mto wa matope. Walimwambia ilikuwa jambo linalositahili kwa sababu halikukuwa hawezi.*
10. Ukoma ni picha ya nini? Na sisi tunapona namna gani?
   *Ukoma ni picha ya dhambi. Ubatizo hutuosha dhambi zetu*.

### Mistari ya kukariri

Yakobo 5:16 – 18; 1 Wafalme 18:38 – 39; Warumi 6:22 – 23

### Mazungumzo

Zungumza vile Mungu wakati mwingine anatumia uwezo mwingi na wakati mwengine anatumia kidogo, na vitu visivyofaa au watu. Mungu anaweza kukutumia namna gani?

### Kuandika

Jifanye kwamba wewe ni Naamani na ueleze vile uliponywa kutoka kwa ukoma.

Haikunyesha kwa zaidi ya miaka mitatu. Mungu alituma Eliya kwa mfalme Ahabu. Eliya aliambia Ahabu kwamba Mungu ataonyesha watu kwamba yeye ni Mungu wa kweli na Baali ni sanamu tu. Ahabu alikusanya watu wote na manabii 450 kwa Mlima wa Karmeli. Eliya aliambia watu waamue kama Mungu au Baali ndiye Mungu wa kweli. Lazima waabudu Mungu wa kweli.

Eliya aliambia manabii wa Ahabu watengeneze madhabahu halafu waweke juu ndama na wasiwashe moto kwa hiyo dhabihu yao. Mungu wa kweli ndiye atatuma moto. Manabii wa Baali waliita Baali, wakimuuliza atume moto. Kwa siku nzima walipaza sauti wakiita lakini hakuna kilichofanyika.

Mwishowe, Eliya aliita watu wote waje kwake. Alijenga madhabahu ya mawe 12 na kuweka juu yake ndama. Aliambia watu wamwage juu ya madhabahu maji mapipa 12. Halafu akaomba, “Bwana Mungu, hebu wajue kwamba wewe ni Mungu wa kweli.” Papo hapo moto ulitoka juu angani na kuchoma ndama na mawe na maji yote. Watu waliogopa na kusema, “Bwana, ndiye Mungu.” Eliya aliambia watu wawaue manabii wote wa Baali. Watu waliamini Mungu tena. Eliya aliomba na Mungu akaleta mvua kwa nchi.

Ahabu alipoambia Yezebeli kwamba manabii wa Baali wote walikuwa wameuwa, alikasirika sana. Aliamrisha Eliya auwawe. Eliya aliogopa na akatoroka. Alichoka na akakaa chini ya mti mreteni, malaika alikuja, akamletea chakula akala. Baadaye alisafiri kwa siku 40 mpaka kwa Mlima wa Horebu. Aliishi kwa pango kando ya mlima. Mungu alimuulza mbona alikuwa pale. Eliya aliambia Mungu ni yeye tu ndiye nabii aliyebaki na alikuwa anatoroka kutoka kwa Yezebeli. Mungu aliambia Eliya asimame kwa mlango wa pango. Pale Eliya aliona mtetemeko wa nchi, upepo mkali wa moto - lakini Mungu hakukuwemo. Halafu akasikia sauti ndogo ya chini. Mungu alikuwa ndani ya hiyo sauti ndogo ya chini. Hii inaonyesha kwamba ingawaje Mungu ni wa nguvu, anaweza kuwa na sisi kwa hali tulivu ya kufariji. Anatulinda kila wakati. Mungu alimwambia Eliya kwamba kuna watu 7,000 Israeli wenye hawakuabudu Baali. Mungu alituma Eliya kwenda kutafuta mtu aliyeitwa Elisha atakayemsaidia. Elisha alisafiri na Eliya wakizunguka, akimsaidia.

Siku moja Mungu akaambia Eliya kwamba ilikuwa imetimia wakati Elisha awe nabii mpya. Eliya na Elisha walienda kwa Mto wa Yordani. Eliya alichukua vazi lake na akapiga maji na maji yaligawanyika na wakavuka kwa nchi kavu. Eliya aliuliza Elisha achague alichotaka kwake. Elisha alijua kwamba ni kazi ngumu kuwa nabii, kwa hivyo akachagua kuwa na nguvu za Mungu maradufu ili zimsaidie. Mungu alimwambia kwamba atapata hizo nguvu kama atamwona Eliya akinyakuliwa.

Kwa ghafula, Elisha aliona gari na farasi za moto angani na Eliya akatoweka kwa upepo wa kisulisuli. Eliya aliangusha vazi lake alipokuwa akienda. Elisha alichukua vazi la Eliya akapiga maji ya Mto wa Yordani. Maji yakagawanyika na Elisha akavuka. Watu wakajua kwamba Elisha alikuwa na nguvu za Mungu na yeye ndiye nabii mpya. Elisha alifanya miujiza nyingi akisaidia watu kujua kwamba Mungu ni Mungu wa kweli. Elisha alisafiri kila mahali akifundisha watu juu ya Mungu, akiwasaidia waamini na kutii amri zake.

Naamani alikuwa nahodha wa jeshi la Siria na alikuwa na ukoma. Watu wa Siria waliishi wakipigana na watu wa Israeli. Kuna wakati walishinda na kuchukua watu wa Israeli mateka. Mke wa Naamani alikuwa na mjakazi mtumwa kutoka Israeli. Huyu mjakazi alikuwa na imani na alipenda mwaajiri wake. Mke wa Naamani alikuwa na huzuni kwa sababu mmewe alikuwa na ukoma. Huyu mjakazi alimwambia kwamba huko Israeli kuna nabii na anauwezo wa Mungu. Anaweza kuponya Naamani ukoma. Naamani aliposikia hivyo, aliuliza mfalme amruhusu aende kumwona huyu nabii. Mfalme alimpa zawadi ili ampelekee nabii Elisha.

Naamani alipofika kwa nyumba ya Elisha, Elisha alimtumia ujumbe, “Enda uoge kwa Mto wa Yordani mara 7.” Naamani alikuwa mtu wa maana sana kwa nchi ya Siria. Naamani hakufurahi kwa sababu Elisha hakutoka inje kumwona. Tena alijua kwamba Mto wa Yordani ulikuwa mto mdogo na matope mengi. Mito Abana na Farpari za Siria ni nzuri kuliko Mto wa Yordani. Angeoga kule akitaka. Naamani alikasika sana na akaanza kurudi kwa hasira nyingi.

Watumishi wake walimsihi. Nabii hajakwambia kufanya jambo kubwa au ngumu. Walimwambia ni rahisi sana kuoga na upone. Kwa hivyo Naamani aliacha kuwa na maringo na kiburi na akaoga kwa Mto wa Yordani. Alipotoka majini baada ya mara ya 7, ukoma ulikuwa hakuna. Ngozi yake ilikuwa imepona.

Naamani alijifunza kuwa mpole na kuamini Mungu. Sasa alikuwa amepona. Alirudi kwa nabii na kumpa zawadi nyingi. Lakini Elisha hakuchukua. Alikuwa ameponywa kwa uwezo wa Mungu sio wa Elisha. Naamani alirudi Siria na kuabudu Mungu kule.

Ukoma ni picha ya dhambi. Sote tunatenda dhambi tena tunakufa. Lakini Mungu ametupa uponyaji. Ametwambia lazima tuoshe dhambi zetu ili tuwe wasafi kwa njia ya ubatizo. Lazima tufanye vile Mungu anasema. Kama Naamani angeoga kwa mito ya Abana na Farpari hangepona kwa sababu hangekuwa ametii Mungu. Lazima tuheshimu Mungu ipazavyo.